JINSI YA KUDESIGN BLOG INAYOLIPA



Makala imechapwa na: said suleman
Phone: 0656 848274
Visit: http://www.networkacademy.ga
Email: shamilysaidi@gmail.com

Habari ya wakati huu wakuu,

Na wakati huo huo nitoe angalizo kwamba usiache kazi yako ya kuajiriwa au kazi nyingine uliyojiajiri na ukahamia kublog ukitegemea utapata hela za kukutosha kuendelea na maisha yako! Ni kweli unaweza kupata pesa kwa kuwa na blog lakini ni jambo linalohitaji muda, miezi kadhaa na hata miaka wakati mwingine mpaka uje uone hela ikitoka kwenye hiyo blog na kuja kwako.

Blog ni nini?

Neno Blog linatokana na maneno mawili ya kiingereza ambayo ni ‘web logs',. Neno ‘Logs' tafsiri yake ni ‘ni kuweka kwenye rekodi'. Hivyo Blog ni aina ya tovuti au website ambayo inaongezwa makala mpya kila mara kwa mpangilio maalumu. Kuna aina kuu 2 za blog, blog za bure na bure za kulipia.

Kwenye makala hii tutajadili zaidi kuhusiana na blog za kulipia sababu ndizo zinazoweza kulipa.

Ili kudesign blog inayolipa unahitaji vitu hivi kwa kuanzia;

1. Top Level Domain (T.L.D)

Domain ni nini?

Domain ni JINA LA BLOG. Hivyo jamiiforums.com au millardayo.com/ yote haya ni majina ya blog au tovuti.

Domain au jina la blog huwa na sehemu kuu mbili, mzizi (jina) na kiambishi tamati (extension)

Hivyo jamiiforums na millardayo haya yote mawili ni sehemu ya mzizi wa jina
na .com ndiyo kiambishi tamati au domain extension kama tulivyozoea

Sasa, top level domain ni domain za namna gani?

Ili uwe na blog inayolipa kitu cha kwanza ni kuwa na top level domain, hizi domain ambazo kwanza hazipatikani bure, ili kuwa nayo ni lazima ununue na mara nyingi unaweza kununua na kuimiliki kwa mwaka mmoja au miwili au hata zaidi kadri utakavyolipia wewe.

Pili, hizi top level domain mara nyingi ni kuwa, mara tu baada ya jina basi kinachofuatia ni kiambishi tamati (extension), mfano jamiiforums baada tu ya jina mwisho ni .com hivyo unasoma jamiiforums.com

Kumbe zile ambazo siyo top level domain kwanza ni bure na unakuwa huna umiliki wake kwa asilimia 100, hivyo unaweza ukaamka tu siku moja na usiione blog yako hewani na ukiuliza utaambiwa inakiuka vigezo na masharti yetu, hata kama si kweli!

Siyo hivyo tu, zile ambazo siyo top level domain huwa pia ni ndefu zaidi kuliko hizi top level domain kwa sababu katika hilo hilo jina lako kutatakiwa kuwepo pia jina la aliyekupa hiyo domain bure au wakati mwingine unaweza ukalazimishwa kiambishi tamati (extension) kiweje.

Hivyo ukitaka kuwa na blog inayolipa sahau kuhusu .blogspot.com, .wordpress.com, .webly.com na mengine mengi kama hayo.

Tuchukulie mfano kama hawa jamiiforums wangeamua kutumia jina la bure kutoka google kwa mfano, jina lao lingekuwa linasomeka hivi => jamiiforums.blogspot.com !!!

Umeona tofauti
ya **jamiiforums.com** na **jamiiforums.blogspot.com**?

Hivyo top level domain kwanza ni fupi na hivyo linakuwa rahisi hata kutamkwa na kukumbukika kirahisi. Ni rahisi kutaja au kutamka jamiiforums.com kuliko kutaja au kutamka na kukumbuka jamiiforums.blogspot.com

Watu wengi wanaotaka kuwa waandishi wa kujitegemea kwenye mtandao (bloggers) wengi hukosea kwa kutumia muda mrefu wakiwa na domain au majina ya blog ya bure. Haidhuru kutumia jina la bure lakini iwe ni kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu tu kwa muda mchache, baada ya muda au hata mwanzoni kabisa kama unataka kuwa na blog inayolipa ni vema kuwa na top level domain mapema. Siyo gharama, top level domain unaweza kuipata

kuanzia Tsh 10000 na haizidi Tsh 30000 labda iwe ni special sana kama zilivyo za .academy

Kwa kifupi unapochagua domain name angalia iyo name iendane na content za blog……mfano

org	organization	Hutumika kwa organization hasa za serikari mfano www.nacte.org Huwezi sema www.nacte.com au www.Tanzaniapolice.org huwezi sema www.tanzaniapolice.com
net	network	Hutumika kwa website za mambo ya network kama cisco na vyuo vya network mfano www.udsm.net www.cisco.net
.info	information	Hutumika kwa website zinazohusika na information
com	commercial	Biashara, blog na website zote zinazofanya biashara huishia na com…..mfano www.mwananchi.com
ml	military	Website za kijeshi..mfano www.jwtz.ml.tz

		Huwezi sema www.jwtz.com.....com
go	government	Hutumika kwa Website za serikari pia Mfano www.tcu.go.tz Huwezi sema www.tcu.com..... Pia inaweza kuwa www.tcu.net Au www.tcu.go.tz yategemea website yahusika na nini
co	company	Hutumika kwa website na blog za makampuni www.azam.co.tz usikariri inaweza ikawa pia www.azam.com maana com ni biashara angalia na azam ashughulika na nini
ac	academy	Vyuo na taasisi za elimu Mfano www.udsm.ac.tz Usikariri udsm ni chuo chaweza husika na network yaweza kua

		pia www.udsm.net Usikariri udsm yaweza kuwa campuni pia yaweza kuwa www.udsm.co.tz

HIZO NI DOMAIN NAME SHARIA ZAKE HIVYO UNAPOCHAGUA DOMAIN NAME ANGALIA BLOG AU WEB YAKO INASHUGULIKA NA NINI KISHA CHAGUA DOMAIN NAME……KUNUNUA DOMAIN NAME HUTUMIKA US DOLLAS….NA UWE MJUZI KIDOGO WA WEBSITE DESIGN KUMBUKA UNAWEZA KUFANYA HOSTING…….HAPO UTACHAGUA DOMAIN COUNTRY

.tz tanzania
.Ke kenya
.uk united kingdom
.ug uganda

VITU VYA KUZINGATIA UNAPONUNUA DOMAIN

Domain au jina zuri la blog lazima liwe na sifa zifuatazo;

1. Liwe Fupi, kwanini liwe fupi? ili iwe rahisi kutamkwa na kukumbukwa

2. Liendane na maudhui ya blog. Mfano unaona jamiiforums limebeba maudhui au malengo ya blog, jamii ni sisi watumiaji wote na forums ndivyo yalivyo majukwaa. Hii si kanuni hasa kwa blog binafsi zile mtu anaweza kuamua kutumia jina lake kamili na ndani yake akaandika lolote analolipenda au kuhusiana na taaluma au kazi

yake.

Mara nyingi nikipata mtu anataka nimshauri kuhusu blog yake afanye nini iende mbele, cha kwanza nawaambia nitajie blog yako, nikiona tu ni jina la bure basi cha kwanza hata kabla sijaitembelea hiyo blog nitakuambia nunua jina.

Hatua ya kwanza katika kuwa na blog inayolipa ni kuwa na blog yenye jina la kulipia na siyo la bure. Na sababu ni nyingi, kwanza linakuwa ni la kwako kwa asilimia 100, unaweza kulifupisha kadri uwezavyo na linakufanya uonekane upo makini na kazi yako.

Kwa leo tuishie hapa, somo litaendelea na sehemu ya pili. Pia mnipe ushauri kama niwe nafungua uzi mpya kwa kila sehemu ya somo au niwe naendelea nayo kwenye uzi huu huu.

sehemu ya pili;

Jinsi ya ku-design Blog inayolipa (Part 2):

Tunaendelea na sehemu ya pili ya somo letu

2. UNIQUENESS (UPEKEE)

Blog inayolipa lazima iwe ni ya kipekee (Unique). Hapa uwe makini kidogo maana hili ndilo lililo mhimu kuliko yote. Kama huwezi kumshawishi mtembeleaji mpya wa blog yako kuiona blog yako ni ya tofauti, nini kitamfanya aendelee kubaki hapo akisoma au arudi tena kesho kuona kama kuna jipya?

Njia pekee ya uhakika ya kuifanya blog yako ni tofauti na blog nyingine ni UPEKEE. Kama hakuna vitu vya kipekee kwenye blog yako usitegemee mtembeleaji wa kwanza au

mpya wa blog yako kurudi tena au kuitafuta tena hiyo blog.

Ninaposema upekee kwenye blog naongelea vitu vikuu viwili ambavyo ni;

1. UNIQUE DESIGN/MUONEKANO WA KIPEKEE

Blog yako ili ilipe lazima iwe na muonekano wa kipekee. Muonekano wake kwa maana ya rangi, menu zake, namna inavyowasiliana na kujibizana na watembeleaji uwe ni wa kipekee na usiobadilika kila mara, mfano leo nimetembelea blog yako nakuta in background ya blue, kesho nakuta ina background nyekundu!, hapana, haiwi hivi. Unaweza kubadili muonekano wa blog yako baada ya miezi 6 au mwaka mmoja au miaka kadhaa, lakini siyo kila mara kwa sababu inaweza hata kuathiri kiasi cha uaminifu wa wasomaji wako kwako.

Hivyo unapofikiria kuanzisha blog yako fikiria pia juu ya kumpata mtengenezaji au designer wa blog atakayekutengenezea blog yenye muonekano wa pekee kwa maana kwamba blog yako haifanani fanani na blog nyingine kirahisi ili kukufanya wa tofauti.

2. UNIQUE CONTENT/MAKALA ZA KIPEKEE ORIJINO

Hapa ndiyo penye shida sana hasa kwa bloggers wengi wa Tanzania. Yaani Bloggers wengi wanachofanya ni kusubiri website ya gazeti fulani au blogger fulani aandike makala na wengine wote wana-copy na ku-paste kwenye blog zao kwa kichwa cha habari kile kile na maelezo yale yale!. Ni vigumu kuwa na blog inayolipa kwa staili hii.

Ili kuwa na Blog inayolipa, blogger unatakiwa ushiriki kwenye

kutayarisha, kuandaa na kuandika makala za blog yako wewe mwenyewe. Sasa kuna sababu gani ya mimi kutembelea blog yako kama makala zako zote una-copy toka blog ya Shigongo?, ni heri nifunguwe kila siku blog ya Shigongo ambako nitapata orijino stori badala ya kuja kwako. Hii inaathari nyingi ikiwemo kukosa traffic kutoka search engines kama vile google.

Kuna vitu vingi sana unavyoweza kuviandika. Lakini wengi wanapenda kuandika tu juu ya mapenzi, michezo na siasa. Unaweza kuandika juu ya somo lolote iwe ni hesabu au biolojia, unaweza kuandika kuhusu kilimo, ufugaji, ujasiriamali, uchumi, afya, utalii, hoteli, shule, saikolojia, ushauri, malezi, na mengine mengi bila idadi na ukaeleimisha jamii inayokuzunguka.

Kwanini watu wanatembelea blog yako? Kwa sababu kuna jambo wanataka kusoma au kujifunza. Ukiwa blogger huna tofauti na mwalimu. Mwalimu au profesa wa chuo kikuu analipwa mshahara kwa sababu kuna kitu fulani anachofundisha.

Anzisha blog, chagua mada maalumu na udumu kwenye mada hiyo ukiifundisha kila mara kidogo kidogo. Andika habari au makala ambayo haifanani na wengine lakini yenye msaada kwa msomaji. Andika jambo likakamilika.

Kuna ushindani mkubwa na unaozidi kuongezeka siku hadi siku kwenye sekta hii ya uandishi. Andika kitu cha pekee (unique story) na mhimu kuliko yote, stori iwe ni yenye kumsaidia au kumuongezea thamani msomaji wako.

Kwa ufupi, sehemu hii ya pili inagusia kwenye jambo la UPEKEE, Upekee kwenye **muonekano** wa blog, *kazi ambayo*

siyo yako wewe blogger bali ni kazi ya msanifu/designer wako na upekee kwenye **makala au stori** zako,*kazi ambayo ni yako moja kwa moja*.

UVIVU ndilo neno pekee linaloweza kusomeka na likaleta maana ukianzia kulisoma upande wowote iwe ni kushoto au kulia.

sehemu ya 3

3. Self Hosted Blog

Ili blog au website ionekane hewani inahitaji vitu viwili

1. Jina (Domain) <= tumeshajadili kuhusu domain hapo juu kwenye TLD
2. stoo/hifadhi Host/Server (Host/Server)

Kama ilivyo kwa majina (domain), kuna majina ya bure na majina ya kulipia na tumeshajadili kwa kirefu hapo juu tofauti ya majina ya bure na majina ya kulipia na tukakubaliana kwamba ili uwe na blog inayolipa, unahitaji uwe na jina la kulipia na siyo la bure na sababu tumezieleza.

Hivyo hata stoo ya kuihifadhi hiyo blog ili ionekane hewani popote duniani zipo za aina mbili, za bure na za kulipia. Kwa kawaida kama ulifungulia blog yako kwenye google na ukabadili jina tu bila kubadili hifadhi (server/host) ya hiyo blog bado unahesabika unatumia stoo ya bure.

Kama ilivyo kwa bloggers wengi wanapoanza kuandika kwenye mtandao wengi huanza au hufikiri kutumia server za bure! Lakini ili upate mafanikio katika hiyo blog unalazimika kuwa na server ya kulipia.

Sehemu ya 3 ya vitu mhimu unavyohitaji ili kuwa na blog inayolipa inajikita kwenye Hosting/Server(Stoo).

Kwanini ulipie server?

Kwa sababu unapata uhuru zaidi na blog yako.

Kwa mfano ukiwa kwenye **server** za bure, mara nyingi

1. Utaambiwa idadi ya watu wanaoweza kutembelea hiyo blog yako kwa siku au kwa mwezi (bandwidth) ni wangapi. Usipolijuwa hili na ukafanya utundu wako siku 1 ukawapeleka watu 1000 au zaidi wakati umeambiwa kwenye hii server ya bure unaweza kuwa na wasomaji 200 tu kwa siku, lazima utaikuta blog yako ipo chini haionekani tena!.

2. Huwezi kuwa na blog yenye uzito (gb) wowote utakao wewe kwa mfano unaweza kuambiwa blog au website yako

isizidi ukubwa wa mb 300 (disc space).

3. Unaweza pia ukaambiwa unaweza kuwa na barua pepe/email 1 au 2 au ukaambiwa huwezi kuwa na barua pepe kwa jina la bog yako mfano ukihifadhi blog yako kwenye google basi email yako haiwezi kuwainfo@fadhilipaulo.com badala yake utalazimika kutumia email ya gmail! <= sasa kama upo makini na kazi yako huwezi kukubali vitu kama hivi.

Lakini yote hayo ni kwa sababu ya bure.

4. Ukiwa kwenye server ya bure wakati mwingine huwezi kujipangia ni mfumo upi utaumia kusanifu (to design) blog yako mfano kama upo kwenye server za google (blogspot) muundo au design ya blog yako lazima iwe ni zile za blogger tu, huwezi kuwa kwenye **blogspot** halafu utumie muundo (design) au mfumo wa blog unaotumia wordpress. Kadharika ukiwa **.wordpress** huwezi kutumia muundo wa blog wa blogger, drupal, joomla na kadharika.

Kumbe ukiwa kwenye server ya kulipia unaweza kuamua mwenyewe blog au website yako iendeshwe kwa mfumo upi ikiwa ni code (html) au utumie mfumo mwingine wowote wa kuendeshea blog (CMS), kama ni wordpress, blogger, html, drupal, Joomla na kadharika na kadharika kadri utakavyo wewe.

Kitu kingine kitakachokugharimu ukiamua kutumia server za

bure ni vile namna ya kuifanya blog yako ionekane kirahisi kwenye injini za kutafutia vitu kwenye mtandao kama vile google, bing, nk. Hili tunaliita Search Engine Optimization (S.E.O), kumbe ukiwa kwenye server ya kulipia unakuwa na namna nyingi ya kulifanikisha hili kirahisi zaidi.

Kwa kifupi ukiwa na server yako ya kulipia kila kitu ni chako, haijalishi muundaji wa website kama ni kampuni au mtu binafsi, unao uwezo wa kufanya lolote kuanzia backups and restoration, kubadili mfumo wa blog wakati wowote na bila kumwambia yeyote.

Binafsi nilitumia server za bure mwanzoni mwa safari hii yangu ya kublog lakini baadaaye niliachana na hizo na nikaanza kulipia baada ya kuona kuna vitu vingi navikosa, kisha idadi ya wasomaji wangu waliendelea kuongezeka hivyo isingewezekana tena kukaa kwenye server za bure au server ndogo ndogo za kulipia.

Kuna server za kulipia za aina nyingi, lakini kabla ya kuamua ununuwe au ulipie ipi inakupasa kwanza kujuwa mahitaji yako na umhimu wa hiyo blog kwako na kwa wasomaji wako. Katika yote, nakushauri ulipie server inayokufanya uwe na ‘Personal Control Panel'. Control Panel (CPanel) ni aina ya mfumo wa kuhifadhia (host/serve) blog au website kwa namna ya pekee, na unapewa vitu vingi vinavyobaki kuwa vyako na unaweza kuiendesha blog au website yako kwa namna au mfumo wowote uutakao.

Labda utakuwa unajiuliza sasa ni bei gani kuwa na stoo/server yako ambayo ni ya kulipia na siyo ya bure? Jibu ni kama lilivyo kwa domain. Ni bei rahisi sana ingawa bei itaongezeka taratibu kadri blog yako inavyokuwa, kwa sehemu kubwa unaweza ukalipia kuanzia 5000 mpaka laki kadhaa au milioni kadhaa kwa mwezi kutegemea na ukubwa wa hiyo blog na ukubwa hapa huwa ni idadi ya watembeleaji na ukubwa wa faili la blog yako ambalo huongezeka ukubwa kadri unavyoandika makala mpya.

Mwishoni kabisa mwa somo hili nitakuambia kabisa wapi ukanunue jina la blog yako na wapi ukanunue stoo ya blog yako.

JINSI YA KUDESIGN BLOG INAYOLIPA sehemu ya 4

4. CONSISTENCE/KUDUMU KWENYE MADA

Hebu fikiria labda ulikuwa ukitafuta somo linalofundisha ‘Namna ya kufuga Mbwa' na unakutana anuani ya blog inayoelezea somo hilo kupitia injini za kutafuatia vitu kwenye mtandao (search engines).

Siku ya pili unarudi kwenye ile blog unakuta kuna masomo ya namna ya kutengeneza keki!. Keshokutwa yake unajaribu kurudi tena uone ni kweli ulichoona jana, mara unakuta post yao ya mwisho inazungumzia namna ya kulima vitunguu swaumu!!!

Hakika, siku ya nne hutarudi tena hapo kutafuta habari juu ya ‘Namna ya kufuga Mbwa'.

Ni vigumu kuwa na blog inayolipa kwa staili ya uendeshaji wa blog wa namna hii.

Fanya blog yako ijulikane ipo hasa kwa ajiri ya nini, wafanye wasomaji wako wawe wazi kujuwa wakija kwako watapata nini.

Blog lazima iwe na mada au topic maalumu moja inayojitambulisha nayo. Blog zipo hasa kwa ajili ya kufundishana jambo au somo fulani moja. Kama ni blog kuhusu michezo, andika habari za michezo, kama inahusu mapenzi, andika mapenzi, kama inahusu biolojia, andika biolojia, kama inahusu teknolojia andika teknolojia, na kadharika na kadharika. Huhitaji kuzungumzia kila jambo kwenye blog yako ili kupata wasomaji wengi na hatimaye ikulipe.

Hizi mada au topic, kwenye ulimwengu huu wa ku-blog huitwa ‘NICHE'.

Kuna NICHE kubwa na niche ndogo ndogo, na kutoka kwenye hiyo niche kubwa bado unaweza kuivunjavunja na kupata kipande kidogo cha sehemu ya hiyo niche kubwa na ikawa ndiyo mada au topic kuu ya blog yako.

Mfano, NICHE KUBWA ni ‘AFYA'. Kutoka niche au mada kubwa au kuu AFYA unaweza kuivunjavunja na ukapata niche ndogo ndogo kama ‘UZITO NA UNENE KUPITA KIASI'. Blog yako kuanzia post ya kwanza hadi ya mwisho zinazungumzia mada moja tu ambayo ni UZITO NA UNENE KUPITA KIASI. Yaani nikihitaji kila kitu kuhusu uzito na unene kupita kiasi basi nikienda blog fulani au blog ya fulani kila kitu kuhusu UZITO NA UNENE KUPITA KIASI nitakipata hapo.

Sasa unakuta blog mara ina post za stori za mapenzi, mara michezo, mara afya, mara teknolojia. Yaani ni vurugu. Blog siyo forum au siyo tovuti ya gazeti. Wewe kama blogger chagua mada moja utakayodumu nayo na watu wakutambuwe kwa hilo.

Kama unapenda magari, blog kuhusu magari. Kama unapenda kilimo, blog kuhusu kilimo, kama unapenda siasa, blog kuhusu siasa, unapenda habari, blog kuhusu habari, unapenda muziki, blog kuhusu muziki …. Na kadharika na kadharika.

Na hii kudumu kwenye mada (being consistent) inahusu vitu viwili kwenye blog, ambavyo ni;

1. **Kudumu kwenye mada au topic ya blog**, (niche). Yaani kama inahusu kilimo basi udumu na masuala ya kilimo na

2. **Kudumu kutoa makala mpya kwa muda na mpangilio maalumu** (persistence). Wasomaji wako watarudi tena na tena kwenye blog yako kama kuna makala mpya kila mara. Hapa JF unaona kuna wasomaji wengi ni kwa sababu kuna mada mpya kila siku na tena ni nyingi maana kila mtu popote alipo anaweza kuanzisha mada tena wakati wowote na mbaya zaidi hao waanzisha mada ni wengi na mada zimepangwa kimajukwaa sababu hii ni forum na siyo blog.

Sasa, sijakushauri ukaanzishe jamiiforum nyingine, wewe kaanzishe blog, dumu kwenye mada ya blog na uandike makala mpya kila mara bila kupumzika. Siyo kila siku! Unielewe hapo. Kama ni blog inayohusu habari, ndiyo unaweza kuandika makala mpya kila siku sababu habari zinatokea kila siku.

Ili kutowachosha wasomaji wako unaweza kufanya makala mpya moja kila baada ya siku 1 au makala mpya 2 kwa wiki. Hii itakusaidia pia kupata traffic toka search engines kama google sababu google anapenda blogs ambazo zinakuwa na makala mpya kila mara (updated) na kwa mpangilio maalumu.

Hii siri nawapa pia website au tovuti za makampuni ambazo website zao ni static na hawana sehemu ya blog kwenye tovuti zao. Kila website sasa inahitaji kuwa na sehemu ya blog

ambako wataandika matukio au elimu yoyote kuhusu huduma zao kila mara ili waweze kupata watembeleaji (traffic) kirahisi kutoka kwenye injini za kutafutia vitu kwenye mtandao (search engines). Itawapunguzia hata gharama zao wanazotumia upande wa masoko (marketing).

Mengine ya haya ninayoyasema hapa yananichoma hata mimi sababu hata mimi nimewahi kukosea staili hii mwanzoni wakati naanza ku-blog kwenye mtandao. Lakini kama elimu na kama kukusaidia wewe usije kupoteza muda na pesa basi uyaepuke ikiwa unataka kutumia mtandao kwa manufaa ya jamii na yako. Kwa maana ya kusanifu (design) na kuwa na blog inayolipa.

Kuna wakati inaweza ikakutokea unao uwezo wa ku-blog au kufundisha mada (niche) zaidi ya moja labda hata 3, yaani mtu ana vipawa vingi Mungu kamjaalia, utafanya nini?. Hapa jaribu, nimesema ‘jaribu' ku-blog kuhusu vyote halafu uone wapi wasomaji wako wanakupenda zaidi na uwekeze muda zaidi upande huo.

Kwahiyo sehemu hii ya nne ya namna ya kudesign blog inayolipa inazungumzia umhimu wa kudumu kwenye mada, ‘CONSISTENCE'. Kudumu kwenye mada inayoitambulisha blog yako (niche) na kudumu kwenye mada kwa maana ya kuleta makala au post mpya kila mara kwa mpangilio maalumu (persistence).

Tutaendelea na sehemu ya 5 ….

Tutaendelea na sehemu ya tano ya somo hili. Tutaenda taratibu walau kila wiki tutapata sehemu 2 za somo hili, hatuna haraka, tunahitaji watu waelewe.

Kwa kuongeza tutaonyesha namna ya kujiunga addsence kwa urahisi kama ikiwezekana na kutumia templates kufanya blog iwe na muonekano wa kuvutia